



JAMHURI YA KENYA

WIZARA YA MAZINGIRA NA MISITU, MABADILIKO YA HALI YA HEWA, NA MISITU

IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA

Dagoretti Corner, Ngong Road, SLP 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya

Simu: 254 (0) 20 3867880-7, 0724 255 153/4

Barua pepe: director@meteo.go.ke, info@meteo.go.ke

Twita: [@MeteoKenya](https://twitter.com/MeteoKenya)

Nambari ya kumbukumbu: KMD/FCST/8-2026/SO/03

Tarehe: 26/08/2026

1. TAARIFA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA KWA MSIMU WA VULI; OKTOBA – DISEMBA 2026

1.1 UTABIRI WA MVUA ZA VULI, OKTOBA-NOVEMBA-DISEMBA 2026

Msimu wa mvua za vuli, (Oktoba–Novemba–Disemba, OND) ni msimu muhimu wa mvua nchini Kenya, hasa katika kaunti za Garissa, Wajir, Mandera, Marsabit, Isiolo, Meru, Tharaka Nithi, Makueni, Kitui, Taita Taveta na Machakos, pamoja na baadhi ya maeneo ya Kajiado na Tana River, ambako mvua za msimu huu huchangia zaidi ya 40% ya jumla ya mvua katika mwaka. Pia, katika baadhi ya maeneo nchini, zaidi ya milimita 700 (mm) za mvua hupokelewa wakati wa msimu huu (Umbo la 1).

Msimu huu huchochewa na Mzunguko wa Ukanda wa kietropiki, (Intertropical Convergence Zone – ITCZ), ambao hupitia mara mbili kwenye inchi yetu, jua likiwa linateremka kutoka Kaskazini kuelekea Kusini (Msimu wa Vuli), na Kusini kuelekea kaskazini (Msimu wa masika). Muda na utendaji wa msimu huu huathiriwa na Dipole ya Bahari ya Hindi (IOD), ambayo husababisha mvua kuwa zaidi ya kiwango cha kawaida maeneo mengi inchini, inapokuwa katika awamu chanya (positive phase). Hali ya El Niño, ambayo kwa sasa ni ya kiwango cha juu, pia huelekeza mvua kuwa ya kiwango cha juu zaidi ya kawaida inapoambatana na IOD chanya (+).

Kwa vipindi vya muda mfupi, yaani wiki mpaka mwezi, kuna kichocheo; Madden–Julian Oscillation (MJO) ambacho ni cha muda mfupi. Kichocheo hiki husababisha mvua kuongezeka wakati kinapokuwa katika awamu zinazofaa. Vile vile, kichocheo kingine ambacho husababisha au kupunguza mvua kwa vipindi vifupi ni vimbunga vya kitropiki katika Bahari ya Hindi. Vimbunga hivi huweza kuelekezea mvua kupunguwa au kuongezeka kulingana na nguvu zake, umbali vilivyo na bara letu au mwelekeo vinaouchukua.

Utabiri unaonyesha kuwa mvua za juu ya wastani zinatarajiwa katika kaunti za Baringo, Bomet, Bungoma, Busia, Elgeyo/Marakwet, Embu, Garissa, Homa Bay, Isiolo, Kajiado, Kakamega, Kericho, Kiambu, Kilifi, Kirinyaga, Kisii, Kisumu, Kitui, Kwale, Laikipia, Lamu, Machakos, Makueni, Mandera, Meru, Migori, Mombasa, Murang'a, Nairobi, Nakuru, Nandi, Narok, Nyamira, Nyandarua, Nyeri, Siaya, Taita/Taveta, Tana River, Tharaka-Nithi, Trans Nzoia, Uasin Gishu, Vihiga, Wajir, pamoja na sehemu kubwa za kaunti za West Pokot, Samburu na Marsabit (Umbo la 2).

Mvua za karibu na wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa kupokelewa katika kaunti ya Turkana na baadhi ya maeneo ya West Pokot, Samburu na Marsabit.

Kulingana na taarifa ya hivi karibuni, tukio la El Niño la mwaka 2026 linaendelea kuimarika katika sehemu ya kati hadi mashariki ya Pasifiki ya Ikweta. Kiashiria cha jadi cha Niño 3.4 kinaonyesha ongezeko la wazi na endelevu, huku wastani wa hivi karibuni wa msimu wa Mei–Julai 2026 ukifikia $+1.51^{\circ}\text{C}$. Thathmini ya mwezi wa Julai pia iliongezeka hadi $+2.03^{\circ}\text{C}$. Aidha, kiashiria cha hivi karibuni cha kila wiki cha Niño 3.4, kilichotabiriwa 12 Agosti 2026, kilifikia $+2.7^{\circ}\text{C}$. Uchunguzi huu unaonyesha kwamba El Niño inaendelea kuimarika zaidi na kuelekea kuwa tukio lenye nguvu zaidi.

Dipole ya Bahari ya Hindi (IOD) kwa sasa iko katika hali ya kawaida (neutral). Kufikia tarehe 23 Agosti 2026, kiashiria cha kila wiki cha IOD kilikuwa $+0.17^{\circ}\text{C}$, ambacho kiko chini ya kiwango cha kuashiria IOD chanya cha $+0.4^{\circ}\text{C}$. Kiwango kinachozidi kiwango hiki kinapaswa kudumu kwa wiki nane mfululizo kabla tukio la IOD chanya halijachukuliwa kuwa limeanzishwa rasmi. Inatarajiwa kuwa kiwango cha sasa cha IOD kitaongezeka na kuvuka kiwango hicho kuanzia Septemba 2026, ingawa bado kuna taswishi kuhusu muda kamili na kiwango cha nguvu ya tukio hilo. Kiwango cha juu zaidi ya IOD kinachotabiriwa kwa msimu huu ni $+0.7$, ambacho kiko karibu zaidi na kiwango kilichoshuhudiwa mwaka 2015 kuliko viwango vilivyorekodiwa mwaka 2023 au 1997.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Kenya (KMSA) itaendelea kufuatilia kwa karibu hali za ENSO na IOD.

2.0 TAREHE ZA MIANZO, KIKOMO NA MGAO WA MVUA ZA VULI, OND 2026

Utabiri wa mianzo, kikomo, na mgao wa mvua za vuli 2026, umetokana na miundo ya kitabiri ya model (dynamical models) pamoja na uchanganuzi wa kitakwimu wa miaka iliyochaguliwa ya usawa (analogue years), ambayo ilionyesha sifa zinazofanana na hali ya mwaka wa sasa.

Mwaka wa usawazisho (analogue years) uliochaguliwa ni 2015, uchaguzi huu ulitoka na tabiri za hivi karibuni za ENSO na IOD. Matokeo ya mvua ya mwaka huo yametolewa kwa marejeleo tu na hayapaswi kutafsiriwa kuwa sehemu ya utabiri wa msimu huu. Badala yake, yanatoa picha ya aina ya matokeo ya mvua inayoweza kujitokeza chini ya hali za jumla za hali ya hewa duniani zinazofanana.

Katika msimu huu, mgao wa mvua katika maeneo mengi nchini unatarajiwa kuwa wa wastani hadi wa kuridisha, isipokuwa maeneo ya Kaunti za Turkana na Samburu ambapo mgao huu unatarajiwa kuwa wa duni hadi wastani, Mianzo na Kikomo cha mvua hizi pia vinatofautiana kimaeneo, tazama jedwali lifuatalo:

Jedwali la 1: Mwanzo wa Mvua, Kikomo na Mgao wake

Kaunti	Mwanzo wa Mvua	Kikomo cha Mvua	Mgao wake
Nandi, Kakamega, Vihiga, Bungoma, Siaya, Busia, Baringo, Nakuru, Trans-Nzoia, Uasin-Gishu, Elgeyo-Marakwet, West-Pokot, Kisii, Nyamira, Kericho, Bomet, Kisumu, Homabay, Migori na Narok	Itaendelea kutoka mwezi wa tisa (Septemba).	Itaendelea mpaka Januari	Wastani hadi mzuri
Nyandarua, Laikipia, Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Kiambu, Meru, Embu, Tharaka-Nithi na Nairobi	Wiki ya pili mpaka ya tatu Oktoba.	Itaendelea mpaka Januari	Wastani hadi mzuri
Machakos, Kitui, Makueni, Kajiado, Taita-Taveta na maeneo ya ndani ya Tana-River.	Wiki ya tatu hadi ya nne Oktoba.	Itaendelea mpaka Januari	Wastani hadi mzuri
Mombasa, Kwale, Lamu, Kilifi na maeneo ya pwana ya Tana River	Wiki ya pili mpaka ya tatu Oktoba.	Wiki ya kwanza hadi ya pili Disemba	Wastani hadi mzuri
Turkana na Samburu	Wiki ya tatu hadi ya nne Oktoba.	Wiki ya kwanza Disemba	Duni hadi wastani
Marsabit, Mandera, Wajir, Garissa na Isiolo	Wiki ya pili mpaka ya tatu Oktoba.	Wiki ya kwanza hadi ya pili Disemba	Wastani hadi mzuri

3. UTABIRI WA HALI YA JOTO, OND 2026

Msimu wa Oktoba-Novemba-Desemba (OND) nchini Kenya kwa ujumla huwa na hali ya joto, ambapo wastani wa joto huanzia takribani 17°C katika Kaunti za Kericho na Uasin Gishu, hadi zaidi ya 30°C (Climatology) katika baadhi ya maeneo ya Kaunti ya Turkana. Hali hii ya joto huchochewa na Mzunguko wa Ukanda wa kietropiki, (Intertropical Convergence Zone – ITCZ), unapotokea Kusini kuelekea Kaskazini au kinyume chake, (umbo la 4).

Msimu huu wa vuli, joto linatabiriwa kuwa la juu kuliko wastani kwenye maeneo mengi inchini, huku uwezekano mkubwa zaidi ukitarajiwa katika kaunti za Kwale, Mombasa, Kilifi, Lamu, pamoja na baadhi ya maeneo ya Tana River, Taita/Taveta na Garissa.

4. ATHARI ZINAZOTARAJIWA KUTOKANA NA MVUA ZA VULI, 2026


Utabiri wa mvua za kiwango cha zaidi ya wastani zinazotarajiwa katika msimu wa vuli 2026 katika mwezi wa Oktoba hadi Disemba zinatarajiwa kuleta athari hasi (-) na pia chanya (+) kwa sekta mbalimbali. Athari kuu ambazo huenda zikajitokeza zitatolewa na wadau wa sekta husika.

Kumbuka: Utabiri huu wa mvua za vuli utumike pamoja na tabiri za hali ya hewa za siku 5, tabiri za wiki, tabiri za mwezi zikifuatanishwa na jumbe fupi boresha, ripoti za ushauri na jumbe za athari Pamoja na tabiri za wiki na mwezi za Kaunti tokea Ofisi za huduma ya hali ya hewa katika kila Kaunti nchini.


Bw. Charles Muga,

KWA NIABA YA, KAIMU MKURUGENZI WA IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA NCHINI KENYA.


5. VIAMBATANISHO




Umbo la 1a: Hali ya mvua ya muda mrefu katika msimu wa Vuli




Umbo la 1b: Mchango wa mvua za msimu wa vuli.



Umbo la 2: Utabiri wa Mvua za Vuli-OND, 2026



Umbo la 3: Hali ya Joto kwa Msimu wa OND kwa kawaida



Umbo la 4: Utabiri wa hali ya Joto katika msimu wa Vuli 2026